



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. BAG/LD/32936/22

Tarehe: 08 Disemba, 2025

Mkurugenzi Mkuu,

Mamlaka ya Uwekezaji na Ukanda Maalum wa Kiuchumi (TISEZA),

S.L.P 938,

DAR ES SALAAM.

**Yah: KUOMBA UTHIBITISHO WA UMILIKI WA KIWANJA NA. 216 KITALU 'Y' ENEO
LA MAPINGA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO.**

Husika na kichwa habari hapo juu.

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo inakiri kupokea barua yako yenye Kumb Na. CB.48/259/01/33 ya tarehe 17 Oktoba, 2025 ya kuomba kuthibitishiwa umiliki na matumizi ya kiwanja tajwa kutokana na Ofisi yako kupokea maombi kutoka Kampuni ya Chai Leo Limited ya kufanya marekebisho ya cheti cha uwekezaji kwa kuongeza eneo tajwa na kulingana na mradi kusudiwa.

3. Ofisi inakufahamisha kuwa, imepokea maombi ya uhamisho wa miliki kutoka kwa wamiliki wa kiwanja tajwa Ndugu Rose Godfrey Muro na Lucyana Godfrey Muro kupitia Hati Na. 19357 PWN kwenda kwa Kampuni ya Chai Leo Limited. Pamoja na maombi yao pia, waliwasilisha nakala ya mkataba wa kuuza kiwanja hicho kwa kampuni hiyo. Ofisi imeshindwa kufanyia kazi maombi yao kutokana na kutowasilisha cheti cha vivutio vya uwekezaji katika eneo hilo kutoka Ofisi yako kwakuwa kampuni hiyo ni ya kigeni.

4. Aidha, wamiliki hao waliwasilisha maombi ya mabadiliko ya matumizi ya kiwanja hicho ili kuendana na mradi unaokusudiwa kufanyika katika eneo hilo kama ulivyoeleza katika barua yako ambapo taratibu za mabadiliko hayo zimekamilika ngazi ya Halmashauri na kuwasilishwa katika Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Pwani kwa barua yenye Kumb. Na. AE 109/475/01/19 ya tarehe 3/12/2025 kwa ajili ya uidhinishaji.

Barua zote ziadikwa kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya Uhindini, S.L.P. 59, 61301-BAGAMOYO. Mkoa wa Pwani. Simu
Na: 0733661575, Nukushik: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz barua@bagamoydc.go.tz Tovuti: www.bagamoydc.go.tz

5. Hivyo, Ofisi haina pingamizi kwa Taasisi yako kuendelea na taratibu za kuongeza eneo hilo la mradi huo kwenye cheti cha vivutio vya uwekezaji kwa Kampuni hiyo katika eneo tajwa. Upatikanaji wa cheti hicho kutawezesha ombi lao la umilikishaji kwa utaratibu za uwekezaji wa kigeni kuendelea.

6. Ahsante.



Shauri Selenda
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO

Nakala:- Mkurugenzi,
Chai Leo Limited,
S.L.P 35,
BAGAMOYO.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO
S.L.P. 59
BAGAMOYO



FORWARD

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya Uhindini, S.L.P. 59, 61301-BAGAMOYO. Mkoa wa Pwani.Simu
Na: 0733860575, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz, barua@bagamoyodc.go.tz Tovuti: www.bagamoyodc.go.tz